**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**
**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **MAJIBU** **Mwaka: 2021**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A,B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali lina alama Nne.

1. Bainisha mambo manne ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa Somo la Kiswahili.
2. Fafanua kwa kifupi sifa nne za mashairi ya kimapokeo.
3. Kuchambua kwa kifupi mambo manne yanayoweza kuharibu zana za kufundishia na kujifunzia.
4. Eleza maana ya istilahi zifuatazo kwa kutumia mifano miwili kwa kila istilahi:
   (a) Sentensi.
   (b) Kishazi
5. Fafanua tofauti nne zilizopo kati ya njia shirikishi na njia shirikishi hafifu.
6. Kwa kutumia mifano miwili kwa kila moja ili kutoa maana ya istilahi zifuatazo:
   (a) Ala tuli
   (b) Ala sogezi
7. Taja sifa nne za muhtasari wa somo la Kiswahili.
8. (a) Toa maana ya ufahamu
   (b) Eleza kwa kifupi aina mbili za ufahamu
9. Taja kazi nne za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.
10. Taja wadau wawili wa elimu kisha kuonesha namna wanavyonufaika na matokeo ya upimaji.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali Mawili katika sehemu hii. Kila swali lina alama 15

11. Tumia ushahidi wa kiisimu kuthibitisha kwamba 'Kiswahili ni Kibantu' huku akitoa mifano anuai kutoka katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.
12. Kwa kutumia hoja tano, onesha namna msanii alivyotumia mbinu ya taswira katika kuibua dhamira mbalimbali kwa kutumia diwani ya KARIBU NDANI.
13. Soma shairi kisha jibu maswali kuhusiana na shairi ulilosoma.

   (a) Pendekeza kichwa kinachoweza kuwa muafaka kwa shairi alilosoma.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

(b) Eleza maana ya "mirija yote kuzibwa" kama ilivyotumika na mshairi katika ubeti wa nne.

(c) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi:
- (i) Shere
- (ii) Kinyama
- (iii) Makupe
- (iv) Mabeberu

(d) Taja na eleza maana ya methali inayoweza kupatikana katika ubeti wa mwisho.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali Mawili katika sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

14. Bainisha uhusiano uliopo kati ya muhtasari na vifaa vingine vya mtaala.

15. Fafanua mbinu tano zinazotumika kusaidia wanafunzi wasioweza kusoma kwa ufasaha katika shule za sekondari.

16. Eleza athari tatu chanya na athari tatu hasi za maswali ya insha katika upimaji kwa mwanafunzi. Athari


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org